HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO.

IMEANDALIWA NA;

MKURUGENZI MTENDAJI (W) LONGIDO - DED +255-0655-268-384

Tofuti ya Halmashauri: www.longidodc.go.tz

Simu: 027-2539603/3

Fax 027-2539603

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 NA BAKAA LA 2018/2019 KWA KUPITIA MAPATO YA NDANI (OS) KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA- JULAI 2019 HADI JUNI 2020 MWAKA WA FEDHA 2019/2020









YALIYOMO


| YALIYOMO | | |
|---|---|---|
| Cover page (Nembo na Anuani ya Halmashauri) | | 1 |
| Picha ya Taarifa mbalimbali | | 2 |
| Yaliyomo | | 3 |
| Utangulizi | | 4 |
| **ORODHA YA MAJEDWALI** | | |
| JEDWLI I: KUONYESHA BAJETI YA HALIMASHAURI MWAKA WA FEDHA 2019/2020. | | 4 |
| JEDWLI II: KUONYESHA UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA FEDHA ZA BAKAA (CARRY OVER) MAPATO YA NDANI MWAKA WA FEDHA 2018/2019 | | 7 |
| JEDWALI III: MATUMIZI YA FEDHA ZA NDANI KATIKA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA I 2019/2020 | | 11 |
| | | |
| **3 ORODHA YA CHATI** | | |
| CHATI I: Kuonyesha Bajeti Kuu ya Halmashauri Mwaka wa Fedha 2019/2020 (Makadirio ya Mapato na Matumizi) | | 4 |
| **4 ORODHA YA PICHA** | | |
| PICHA I:WANANCHI JAMII YA KIMASAI LONGIDO WAKIWA KATIKA MKUTANO WA KUJADILI MPANGO WA MAENDELEO WA WILAYA 2019/2020 | | **6** |
| **UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KUPITIA FEDHA ZA BAKAA ZA MWAKA WA FEDHA 2018/2019** | | **6** |
| PICHA II:KATIBU MKUU TAMISEMI AKIWA NA KATIBU TAWALA ARUSHA,DC NA MKURUGENZI LONGIDO AKIKAGUA UJENZI WA KITUO CHA AFYA EWORENDEKE WILAYANI LONGIDO | | **8** |
| PICHA III: MWONEKANO KITUO CHA AFYA EWORENDEKE | | **9** |
| PICHA IV: KATIBU MKUU TAMISEMI AKIWA KITUO CHA ENGARENAIBOR | | 10 |
| PICHA V: KATIBU MKUU TAMISEMI AKIWA VIONGOZI WENGINE KATIKA KITUO CHA ENGARENAIBOR | | 11 |
| PICHA VI: MKUU WA WILAYA LONGIDO AKIKABIDHI KWA WAJASIRIAMALI MFANO WA HUNDI TSHS.50,000,000 | | 13 |
| VII:WAJASIRIAMALI WAKIONYESHA BIDHAA ZA BATIK KUTOKANA NA MIKPO NAFUU ITOLEWAYO NA HALMASHAURI | | 14 |
| PICHA VIII :KATIBU MKUU TAMISEMI AKIONYESHWA BIDHAA ZA MIKATE KATIKA KIWANDA CHA MIKATE NAMANGA KWA MIKOPO YA WAJASIRIAMALI | | 15 |

| | | |
|---|---|---|
| PICHA IX :JAMII YA WAFUGAJI WAKIWA KATIKA MKUTANO WA HADHARA | | 16 |
| 6 CHANGAMOTO MBALIMBALI | | 16 |
| 7 UTATUZI WA CHANGAMOTO | | 17 |


## UTANGULIZI

Katika mwaka wa fedha **2019/2020** Halmashauri imepanga kukusanya na kutumia, **Tshs.18,522,037,097,** kama bajeti ya Halmashauri kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Juni 2020.

**JEDWLI I: KUONYESHA BAJETI YA HALIMASHAURI MWAKA WA FEDHA 2019/2020.**

| NA | KIFUNGU CHA BAJETI 2019/2020 | MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA KILA KIFUNGU | ASILIMIA YA KIFUNGU KATIKA BAJETI |
|---|---|---|---|
| 1 | MISHAHARA (PE) | 10,825,886,497 | 58.45 |
| 2 | MIRADI YA MAENDELEO(DEV.) | 5,151,058,000 | 27.81 |
| 3 | MATUMIZI MENGINEYO (OC) | 616,669,000 | 3.33 |
| 4 | MAPATO YA NDANI (OS) | 1,928,423,600 | 10.41 |
| 5 | **JUMLA KUU YA BAJETI 2019/2020** | **18,522,037,097** | **100** |

Mgawanyo wa matuimizi ya fedha za bajeti 2019/2020 ni kama ifuatavyo:


i) Mishahara Personal Emolument (PE) 10,825,886,497 (58.45%)

**ii)** Miradi ya Maendeleo (Development Budget) 5,151,058,000 (27.81%)

iii) Matumizi ya kawaida ( Other Charges -OC) 616,669,000 (3.33%)

iv) Mapato ya ndani ( Own Source ) 1,928,423,600(10.41%)

**JUMLA 18,522,037,097**




*CHATI I: Kuonyesha Bajeti Kuu ya Halmashauri Mwaka wa Fedha 2019/2020 (Makadirio ya Mapato na Matumizi)*




PICHA 1:*WANANCHI JAMII YA KIMASAI LONGIDO WAKIWA KATIKA MKUTANO WA KUJADILI MPANGO WA MAENDELEO WA WILAYA 2019/2020*

Katika robo ya kwanza **2019/2020** Halmashauri ilitekeleza miradi ifuatayo kwa fedha za bakaa (carry over fund) toka mwaka wa fedha **2018/2019:**

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KUPITIA FEDHA ZA BAKAA ZA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

Katika kipindi hiki Halmashauri ilitekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za Bakaa toka mwaka wa fedha **2018/2019** yatokanayo na mapato ya ndani kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapo chini.Jumla ya **Tshs.38,203,972** kati ya **Tshs. 58,168,994**

**JEDWLI II: KUONYESHA UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA FEDHA ZA BAKAA (CARRY OVER) MAPATO YA NDANI MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

| NA | BAKAA 2018/2019 | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | KAZI ZILIZOFANYIKA | % YA MATUMIZI | MAELEZO/MAONI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 5,273,248 | 5,273,248 | 1,400,000 | Kununua projector na komputa Ofisi ya Mipango | **26.55** | Ununuzi wa komputa 1 utafanyika robo ya pili (II) |
| 2 | 20,214,774 | 20,214,774 | 4,123,000 | Kuweza ujenzi wa madarasa Sekondari ya Lekule | **35.24** | Mkandarasi TRANSGEOTEK na TEVIENDA wako site kwaajili ya ujenzi |
| 3 | 5,600,000 | 5,600,000 | 5,600,000 | Kukamilisha ujenzi wa mifereji ya maji katika Jengo la Halmashauri | **100.00** | Kazi imekamilika |
| 4 | 2,762,155 | 2,762,155 | 2,762,155 | Kukamilisha ujenzi wa Madarasa Tingatinga Sekondari | **100** | Ujenzi umekamilika |
| 5 | 3,318,817 | 3,318,817 | 3,318,817 | Kuwezesha ujenzi wa Kituo cha Afya Engarenaibor | **100** | Ujenzi unaendelea |
| 6 | 2,000,000 | 2,000,000 | 2,000,000 | Kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Afya Eorendeke | **100** | Ujenzi unaendelea |
| 7 | 19,000,000 | 19,000,000 | 19,000,000 | Kukamilisha ufungaji wa X-ray katika Kituo cha Afya Longido | **100** | Utekelezaji unaendelea |
| | **58,168,994** | **58,168,994** | **38,203,972** | | | |

Katika kipindi cha robo ya kwanza miradi iliyotekelezwa kwa fedha za bakaa ni miradi ya:

**Afya**

Ufungaji wa mashine ya x-ray kituo cha Afya Longido (**Tshs.19,000,000**),kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya Eworendeke(**Tshs.2,000,000)** na Engarenaibor**(Tshs.3,318,817**) kama inavyoonekana katika jedwali **Na.II**

*PICHA II:KATIBU MKUU TAMISEMI AKIWA NA KATIBU TAWALA ARUSHA,DC NA MKURUGENZI LONGIDO AKIKAGUA UJENZI WA KITUO CHA AFYA EWORENDEKE WILAYANI LONGIDO.*





*PICHA III: MWONEKANO KITUO CHA AFYA EWORENDEKE*



*PICHA IV: KATIBU MKUU TAMISEMI AKIWA KITUO CHA ENGARENAIBOR*



PICHA V: KATIBU MKUU TAMISEMI AKIWA VIONGOZI WENGINE KATIKA KITUO CHA ENGARENAIBOR

## Sekondari

Katika eneo la Sekondari miradi ya ujenzi wa madarasa katika Shule ya za Sekondari Lekule **(Tshs.4,123,000**) ulifanyika katika robo ya Julai – Septemba 2019

## Mipango

Katika Idara ya Mipango utekelezaji wa miradi ujenzi wa mifereji ya maji katika jengo la Halmashauri(**Tshs.5,600,000)** umefanyika,ununuzi wa projekta na komputa 1**( Tshs.5,273,248)**

## UTEKELERZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KUPITIA FEDHA ZA MAPATO YA NDANIA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Kwa upande wa mapato ya ndani Halmashauri imepanga kukusanya na kutumia jumla ya **Tshs.1,928,423,600** kama makusanyo ya mapato ya ndani kwaajili ya utekelzaji wa shughuli mbalimbali za Halmashauri.

Katika robo ya Kwanza**(I),** mwaka wa fedha **2019/2020** Halmasahauri ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya **Ths. 501,073,225/** kutoka mapato ya ndani kugharamia shughuli mbalimbali katika Halmashauri(mishahara,miradi ya maendeleo,matumizi mengineyo na mfuko wa Wanawake,Vijana na Walemavu).

Katika kipindi cha robo hii Halmashauri kupitia mapato ya ndani iliweza kutumia jumla ya **Tshs.97,923,225/** katika miradi mbalimbali kutokana na makusanyo **ya Tshs. 501,073,225** ya robo ya kwanza.

**Aidha katika kipindi cha robo ya kwanza Halmashauri** ilitumia **Tshs.58,168,994.** kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na Fedha za bakaa za mwaka wa Fedha **2018/2019**

JEDWALI III: MATUMIZI YA FEDHA ZA NDANI KATIKA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA I 2019/2020

| NA | 2019/2020 | LENGO/MPANGO | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | KAZI ZILIZOFANYIKA | % YA MATUMIZI | MAELEZO/MAONI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 120,000,000 | Kutoa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake,Vijana na Watu wenye Ulemavu. | 120,000,000 | 50,000,000 | Kutoa mikopo kwa vikundi 17 vya Wanawake,Vijana na Watu wenye ulemavu | 42 | Vikundi vingine vya makundi haya vitapatiwa mikopo nafuu katika robo ya II, III na IV |
| 2 | 80,000,000 | Ujenzi wa maabara(Scientific laboratories) katika Shule ya Sekondari Matale | 47,923,225 | 47,923,225 | Kazi ya kupauwa majengo 3 ya maabara umefanyika | 59.9 | Kazi ya ujenzi wa maabara 3 unaendelea. |
| | 200,000,000 | | **167,923,225** | **97,923,225** | | | |

## SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

Idara hii iliweza kutekeleza jukumu lake la uwezeshaji kwa kutoa mikopo nafuu kwa Vikundi 17 vya Wanawake,Vijana na Watu wenye Ulemavu kiasi cha Tshs.**50,000,000/.**Mikopo mingine itaendelea kutolewa katika robo ya **II**

**PICHA VI: MKUU WA WILAYA LONGIDO BWANA AKIKABIDHI KWA WAJASIRIAMALI MFANO WA HUNDI TSHS.50,000,000**





*PICHA VII:WAJASIRIAMALI WAKIONYESHA BIDHAA ZA BATIK KUTOKANA NA MIKPO NAFUU ITOLEWAYO NA HALMASHAURI*

## *ELIMU SEKONDARI*

Katika kipindi hiki Halmashauri imetumia **Tshs.47,923,225** kwaajili ya ujenzi wa majengo ya maabara katika Shule ya Sekondari Matale

Miradi ambayo haikupata fedha kipindi hiki itapatiwa fedha katika robo zinazofuata



PICHA VIII :KATIBU MKUU TAMISEMI AKIONYESHWA BIDHAA ZA MIKATE KATIKA KIWANDA CHA MIKATE NAMANGA KWA MIKOPO YA WAJASIRIAMALI




PICHA IX :JAMII YA WAFUGAJI WAKIWA KATIKA MKUTANO WA HADHARA

## 5.0 CHANGAMOTO MBALIMBALI.

- Ufinyu wa vianzo vya mapato.
- Kuwepo kwa kadi za wafanyabiashara ndogondogo
- Mwitikio waJamii katika kuchangia miradi ya maendeleo bado mdogo.
- Watumishi wachache katika Idara mbalimbali mfano katika Idara ya fedha mahitaji ya Watumishi ni 12 lakini waliopo ni 7(saba tu).
- Kutokuwepo mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi katika Idara ya fedha na mipango
- Kuwepo kwa sheria na taratibu zaukusanyaji wa mapato zinazokinzanzan.
- Maagizo toka Serikali kuu ambayo yanzuiya ukusanyaji wa mapato katika vianzo kadhaa.mafnno Halmashauri hairuhusiwai kukusanya ushuru kwa mazao yasiozidi tani moja
- Gharama kubwa ya ukusanyaji wa mapato

## 5.1 SULUHISHO KWA CHANGAMOTO HIZO.

- Kuendelea kubuni vianzo vipya vya ushuru na mapato
- Kupunguza gharama za ukusanyaji mapato.
- Kuweka bajeti ya kuajiri watumishi wapya.
- Kuandaa na kutoa mafunzo mbalimbali kwa Watumishi wa Halmashauri.
- Kuhamasiha Jamii juu ya umuhimu wa kuchangia miradi ya maendeleo
- Kushirikiana na wadau mbalimbali wa Halmashauri katika kutoa mafunzo,mifumo,fedha na utaalamu kwa watumishi wa Halmashauri.
- Kuongeza motisha kwa Wakusanyaji mapato ya Halmashauri.

## MIRADI AMBAYO HAKUTEKELEZWA/HAIKUPATIWA FEDHA KATIKA ROBO YA I 2019/2020

Miradi ifuatayo hakupata fedha katika kipindi cha robo ya kwanza (I) 2019/2020 na ambayo itapatiwa fedha za utekelezaji katika robo ya II nikama ifuatavyo:-

### AFYA

- Kukamilisha chumba cha X-ray katika Kituo cha Afya Longido - **28,440,000**
- Kuwezesha ujenzi wa Kituo cha Afya Leremeta - **30,000,000**
- Kukamilisha ujenzi wa nyumba ya Mtumishi katika Zahanati ya Matale - **30,000,000**
- Ununuzi wa vifaa katika katika Ofisi ya Katibu wa Afya - **2,000,000**

### MIPANGO NA UFUATILIAJI

- Kukamilisha miradi 5 iliyoibuliwa na wananchi(Community initiated projects) - **112,010,000**
- Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini katika Vijiji 49 - **9,700,000**
- Kuandaa maandiko ya miradi Mkakati - **17,000,000**
- Kukusanya Takwimu za Wilaya na Halmashauri katika Kata 18 - **2,150,000**
- Kuandaa sera ya kupambana na Majanga ya Wilaya Longido - **5,850,000**

**MIFUGO NA UVUVI**

- Kufanya ukarabati wa Sehemu ya Machinjio Namanga - **15,000,000**
- Kushiriki maonyesho ya NaneNane Kanda ya Kaskasini - **10,000,000**

**KILIMO NA UMWAGILIAJI**

- Kushiriki maonyesho ya NaneNane Kanda ya Kaskasini **- 12,000,000**

**UTAWALA**

- Kununua gari la Mkurugenzi Mtendaji - **140,000,000**